TANGAZO LA SERIKALI NA.75 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MBAMBO YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Mbambo ya mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 125 yenye majira-nukta 586832MS, 8968321KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki mwa mji wa Mbambo katika uelekeo wa KS $15^0$ 13' 47.04 MS kwa umbali wa kilomita 2.77 hadi kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 587560MS, 8965647KZ;

baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS $79^0$ 09' 15.12 MG kwa umbali wa kilomita 0.22 hadi kwenye alama ya mpaka namba B yenye majira-nukta 587346MS, 8965606KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi mwa ziwa Ikambangunguru katika uelekeo wa KS $89^0$ 29' 44.34 MG kwa umbali wa kilomita 0.57 hadi kwenye alama ya mpaka namba C yenye majira-nukta 586778MS, 8965601KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ $37^0$ 56' 03.54 MG kwa umbali wa kilomita 1.27 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba RG 69 yenye majira-nukta 585997MS, 8966603KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea katika uelekeo Kaskazini-Mashariki mwa Mto Mbaka katika uelekeo wa KZ $0^0$ 56' 35.00 MS kwa umbali wa kilometa 1.21 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 122 yenye majira-nukta 586017MS, 8967818KZ;baada ya hapo unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ $22^0$ 01' 01.23MS kwa umbali wa kilomita 0.59 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira-nukta 586239MS, 8968367KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki mwa ziwa Itende katika uelekeo wa KS $85^0$ 33' 51.67 MS. kwa umbali wa kilomita 0.59 hadi kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba VMA 125 yenye majira-nukta 586832MS, 8968321KZ unapoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*